# WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA

JARIDA LA MTANDAONI I AGOSTI 2022





"Wananchi lindeni na kuutunza Kituo cha pamoja cha forodha mipakani (OSBP) Kasumulu kati ya Tanzania na Malawi kwa maslahi mapana ya Taifa."

Limeandaliwa na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara

uwekezajiviwandabiashara | www.mit.go.tz




# Rais Samia Awataka Wananchi Kulinda Mali za Umma

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amewaasa wananchi kuulinda na kuutunza mradi wa Kituo cha pamoja cha forodha mipakani (OSBP) Kasumulu  ili uwe endelevu kwa maslahi mapana ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

Ameyasema hayo alipokuwa akiweka  Jiwe la Msingi la Ujenzi wa Kituo cha pamoja cha Forodha Mipakani (OSBP) Kasumulu Wilayani Kyela Mkoani Mbeya mpakani mwa Tanzania na Malawi Agosti 07, 2022.

Aidha, ametoa  pongezi kwa waliojenga mradi huo huku akisema ni matumaini yake kwamba atarudi kwa ajili ya kuuzindua ili uanze kuhudumia wananchi.

“Ombi langu naomba wananchi muulinde, mradi huu ni wenu,naomba mtoe ushirikiano ,ulindeni pamoja na miundombinu yake ili ukae kwa kipindi kirefu na uweze kuchangia maendeleo ya Taifa letu.”amesisitiza Rais Samia

Awali akitoa maelezo kwa Mhe. Rais Samia, Mtendaji Mkuu wa TBA, Arch. Daudi Kondoro amesema ujenzi huo unajumuisha eneo la maegesho ya magari ambalo lina uwezo wa kuchukua Mabasi 18, magari madogo 22. Pia kuna eneo la maegesho ya malori.

Amefafanua kuwa mradi huo pia unahusisha jengo la abiria lenye sehemu za kukagua mazao na bidhaa nyingine. Pia kuna sehemu za usalama kwa ajili ya kupima afya za abiria na endapo itabainika kuna mgonjwa, ipo sehemu ya Karantini ya kumhifadhi mgonjwa huyo kwa muda.

Wananchi waliohudhuria hafla hiyo, wameshukuru na kupongeza ujenzi huo kuwa utachochea maendeleo katika kwa kiasi kikubwa.

Ujenzi wa Kituo hicho ni jitihada zinazofanywa na Serikali ya awamu ya sita katika kurahisisha ufanyaji Biashara baina ya nchi zinazopakana na Tanzania.

Mradi huo unaojengwa na Kampuni ya China Geo-Engineering Corporation (CGC) na kusimamiwa na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kwa kushirikiana na Kampuni ya Engineering Consultant Group (ECG) kutoka Misri.

# Rais Samia Atembelea Kiwanda cha TANWAT Mkoani Njombe

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan Leo tarehe 10 Agosti, 2022 ametembelea kiwanda Cha Tanganyika Wattle Company Limited (TANWAT) na kuzungumza na wananchi wa Mkoa wa Njombe.

Kiwanda Cha TANWAT Kinajihusisha na uzalishaji wa nguzo za umeme, Dawa ya kutibu Ngozi (Tanin), plywood, mbao na umeme Megawatt 2 ambapo 0.7 Megawatt wanatumia wenyewe na Megawatt 1.3 wanauza kwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na kiwanda hiki kimeajiri wafanyakazi wakudumu 1300.

Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amezungumza na wananchi wa Mkoa wa Njombe na kuwataka kuendeleza ushirikiano kwa uongozi wa Mkoa na Wilaya ili mambo yaendelee kuwa mazuri zaidi.

Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan amewashukuru viongozi wote kwa kazi nzuri ya kukusanya mapato, kuna uwezekano wa kukusanya zaidi, hivyo kuwataka kuongeza juhudi ya kukusanya mapato ili Serikali anayoiongoza iendelee kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan amesema kuwa Kwa Sasa tuko katika maandalizi ya awamu ya pili ya filamu ya Royal tour itakayoitwa "The hidden Tanzania" ikiwa na lengo la kutangaza maeneo mengine yenye vivutio vya utalii vilivyomo nchini Tanzania.



Mhe. Rais Samia ameongeza kwa kusisitiza wananchi kuhesabiwa katika Sensa ya Watu na Makazi ili wananchi kupata huduma kwa idadi ya watu waliopo.

Aidha, Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji amesema kuwa mradi wa Liganga na Mchuchuma ni mradi wa kimkakati na imegundulika kuwa Kuna aliyekuwa akijiita Muwekezaji sio Mwekezaji hivyo tutamuondoa.

Mhe. Dkt. Kijaji amesisitiza kuwa Serikali inahitaji Mwekezaji makini na mahiri atakayetunufaisha Watanzania.

Mhe. Dkt. Kijaji amemaliza Kwa kusema kuwa tayari tumepata Mwekezaji katika Mradi wa Maganga Matitu ambapo mkataba tutakaoingia kwenye mradi huu ni mkataba huru ambao Mwekezaji akishindwa ataondolewa.

Suala la kupanda kwa bidhaa za sabuni, hii imetokana na nchi ya Indonesia kuweka zuio la kuuza nje (export ban) malighafi hiyo ya kutengeza sabuni na kwa maana hiyo ikapelekea kupanda kwa bei. Hata hivyo tumeongea na wenye viwanda na kuahidi kuwa bei itapungua kwa sababu kwa sasa Indonesia imeshafungua soko (removing ban), na sasa wameahidi kuwa ifikapo mwezi Septemba bei inaweza kupungua.

# Rais Samia Aahidi Kiwanda cha Parachichi Iringa

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan ameahidi ujenzi wa kiwanda cha kuchakata parachichi katika mkoa wa Iringa ili kuliongezea thamani zao hilo.

Akizungumza na wananchi wa eneo la Nyololo baada ya kuanza ziara yake ya siku tatu mkoani Iringa, leo Alhamisi Agosti 11, 2022 akitokea Mkoa wa Njombe, Raisi Samia amesema kiwanda hicho kinajengwa kutokana na maombi aliyokuwa amepewa.

"Najua Iringa na Njombe ni wakulima wa maparachichi, kile kiwanda ambacho mbunge aliomba kisimamishwe kinabaki hapa. Na kule Njombe wameomba cha kwao tutawajengea," amesema Rais Samia.

Amesema lengo ni kusafirisha zao hilo nje ya nchi likiwa limeongezewa thamani.

"Lengo ni kusafirisha maparachichi mengi zaidi yenye hadhi nzuri ili tupate pesa nyingi zaidi," amesema Rais Samia.

Baadhi ya wakulima wa parachichi wamesema ujenzi wa kiwanda hicho utaondoa hofu ya kukosekana kwa soko la zao hilo hapo baadae.

Amesema, kutokana na muamko mkubwa wa wakulima wengi kuwekeza kwenye zao hilo, walikuwa na hofu ya kuja kuyumba kwa soko siku za usoni.

"Kama kiwanda kitajengwa kilimo cha zao hili kitaendelea kustawi, binafsi niliogopa labda lingekuja kuyumba kwa sababu kila mtu analima parachichi. Tunashukuru kwa ahadi hii," amesema Inocent Kalinga, mkulima wa Parachichi wilayani Mufindi.



# Serikali Yaeleza Hatua za Kudhibiti Upandaji wa Bei za Bidhaa Muhimu



Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb) ameeleza hatua zinazochukuliwa na Serikali ili kuwapunguzia Wananchi athari zitokanazo na kupanda kwa bei ya bidhaa muhimu.

Dkt. Kijaji ameyasema hayo Agosti 15, 2022 Jijini Dodoma wakati alipokuwa akiongea na waandishi wa habari kuhusu tathmini ya mwenendo wa bei ya bidhaa muhimu Nchini ambapo Wizara inashirikiana na Tume ya Ushindani (FCC) na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kutekeleza jukumu la kufuatilia na kufanya tathmini ya mwenendo wa bei za bidhaa muhimu nchini.

Dkt. Kijaji amesema kuwa hatua hizo ni pamoja na kuwapunguzia gharama za uzalishaji, uagizaji na usambazaji wa bidhaa ili kuleta uhimilivu wa bei kwenye soko lengo likiwa ni kumlinda mlaji kwa kuhakikisha anapata bidhaa bora kwa bei stahiki na kuzuia upandishwaji holela wa bei ya bidhaa mbalimbali.

"Matokeo ya tathmini zilizofanyika hivi karibuni yalionesha kuwa kuna uhimilivu mkubwa wa bei kwa bidhaa zinazozalishwa hapa nchini, ambazo zilionesha ongezeko dogo la bei ikilinganishwa na bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi ambazo zilionesha ongezeko kubwa zaidi la bei. " Amesema Dkt. Kijaji.

Serikali ya awamu ya sita chini ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, imefanya jitihada kubwa za kuweka mazingira rafiki ya ufanyaji biashara nchini, kwa kuchukua hatua mbalimbali katika kudhibiti ongezeko la bei ya bidhaa ikiwa ni pamoja na udhibiti wa upandishwaji holela wa bei za ndani na soko la Dunia .Ameongeza.

kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa wazalishaji wa mbolea kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kuwapunguzia wakulima gharama za uzalishaji na hivyo kuleta unafuu wa bei ya mazao muhimu ya chakula pamoja na kupunguza ushuru kwa maroli yanayosafirisha bidhaa.

Amesema katika sekta ya zao la Ngano Serikali inatekeleza Mkakati wa kuongeza uzalishaji wa zao hilo nchini ili kukabiliana na upungufu wa tani 800,000 wanazoagiza kila mwaka huku kiasi kikubwa kikitoka katika nchi za Urusi na Ukraine.

"Wizara yetu ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara inaunga mkono jitihada za Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan za kuifungua nchi, kuvutia uwekezaji na utalii kwa kutafuta masoko ya bidhaa zinazozalishwa nchini na tayari tumepata matokeo ambapo kwa mwezi Agosti, 2022, fursa mbalimbali zimepatikana katika masoko ya Kimataifa" Amesema Dkt. Kijaji.







# Dkt. Kijaji Ahamasisha Utalii Nyanda za Juu Kusini

Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb) amewaasa viongozi wa Mikoa, Wilaya katika Mkoa wa Mbeya kutumia vyema fursa ya utalii zilizofunguliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kupitia filamu ya Royal Tour.

Dkt. Kijaji aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa filamu ya Royal Tour nyanda za juu kusini pamoja kuzindua makala ya vivutio vya utalii vinavyopatikana katika Mikoa iliyopo nyanda za juu kusini katika ukumbi wa Eden Highlands Hotel uliopo jijini Mbeya.

Dkt. Kijaji alisema kuwa Serikali imetumia nguvu kubwa kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini lakini baadhi ya viongozi pamoja na watumishi walioko katika sekta ya utalii hutumia lugha isiyo faa kwa wageni hivyo kuwafanya kutorudi tena nchini.

Dtk. Kijaji alisistiza Tanzania imejiwekea mkakati wa kuongeza idadi ya watalii kutoka milioni 1.5 hadi kufikia watalii milioni 5 mwaka 2025.

Aliongeza kwa kusema "Kabla ya janga la Covid-19 Tanzania mwaka 2018 ilikua inaingiza kiasi cha dola za kimerekani 2.4 kutoka kwa watalii milioni 1.5 waliokuwa wakitembelea vivutio mbalimbali vya utalii, na inakadiriwa ifikapo mwaka 2025 idadi ya watalii kuongezeka kufikia milioni tano ambao wataingiziza jumla ya bilioni 6".

Dkt. Kijaji pia alitoa wito kwa wadau wa utalii kuendelea kuhamasisha filamu ya Royal Tour na kutangaza vivutio vilivyopo katika Mikoa saba ya Nyanda za juu kusini ambayo ni Mbeya, Iringa, Njombe, Ruvuma, Songwe, Rukwa na



# Serikali Yaahidi Kuendelea Kuzisimamia TANTRADE Kufungua Milango ya Kibiashara

Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb) ameihakikishia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuwa Wizara itaendelea kuisimamia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (TANTRADE) ili iweze kuendelea kufungua milango ya kufanya biashara kati ya Tanzania na Nchi za Afrika Mashariki.

Dkt. Kijaji ameyasema Septemba 1, 2022 jijini Dodoma wakati akiwasilisha taarifa ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kuhusu hali halisi iliyopo katika urali wa biashara kati ya Tanzania na nchi za Afrika Mashariki.

Dkt. Kijaji ameongeza kuwa Tanzania imefungua milango ya kufanya biashara na nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki ikwemo Jamhuri ya Kidemokrasia ya watu wa Congo (DRC) ambayo imekuwa mwanachama mpya katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

"Wizara yangu inatambua vikwazo mbalimbali vya kibiashara vinavyoonekana kero katika ukuaji wa uchumi kwa haraka kati ya wafanyabiashara wa Tanzania na Wafanyabiashara wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) nimepokea maelekezo yote na ushauri wa kamati na naahidi kuufanyia kazi kama mlivyoelekeza" Amesema Dkt. Kijaji.

Naye Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Viwanda, Biashara na Mazingira Mhe. Boniphace Mwita Getere amemshukuru Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa wasilisho zuri lenye lengo la kuondoa tozo na vikwazo visivyo vya lazima vinavyochagia kudumaza ukuaji wa uchumi wa nchi yetu na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

"Nachukua fursa hii kukushukuru wewe Waziri na watendaji wote walio chini yako kwa kazi nzuri mnayofanya, kamati imefurahishwa na ahadi yako ya kushirikiana na mamlaka za kikodi na vikwazo vya njiani hasa mipakani, hii itasaidia kufungua milango kwa wawekezaji wengi kutoka katika jumuiya yetu ya Afrika Mashariki" Amesema Mhe. Getere.

Wakichangia kwa nyakati tofauti wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Viwanda, Biashara na Mazingira wameiambia Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na TANTRADE iwe na utaratibu wa kukutanisha wafanyabiashara wa mipakani wa pande zote mbili za nchi husika, kuwe na vikao vya pamoja na semina zenye lengo la kutoa Elimu ya uwelewa wa tozo na kodi zisizo na kero.



Aidha wameongeza kwa kushauri Wizara kupunguza uuzaji wa malighafi nje ya nchi badala yake ziuzwe bidhaa zilizosindikwa na viwanda vyetu ili kuingizia nchi fedha za kigeni zitakazosaidia kuongeza thamani ya fedha yetu ya ndani.

Kiko hicho ni mwendelezo wa vikao vinavyoendelea vya kamati ya kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira vinavyotarajia kufikia tamati tarehe 10 Septemba, 2022.









# Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira Yaipongeza WMA kwa Utendaji Kazi

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira imeipongeza Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa kazi nzuri inayofanywa na Wakala wa Vipimo nchini (WMA) ya kusimamia sheria za vipimo mbalimbali hapa nchini.

Hayo yamesemwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira Mhe. David Mwakiposa Kihenzile (Mb) katika kikao cha kupokea taarifa ya utendaji kazi ya Wakala wa Vipimo (WMA) mapema Septemba 31, 2022 jijini DODOMA.

"WMA wanafanya kazi kubwa sana ya kumlinda mkulima asipunjwe bidhaa zake wakati wa kuuza na kumlinda mlaji asipunjwe kwa kuuziwa kilo za bidhaa zizizostahili" Amesema Mhe. Kihenzile.

Aidha wajumbe wa kamati hiyo wakichangia kwa nyakati tofauti wametoa maoni na mapendekezo mbalimbali wakiomba wizara kupitia WMA kuongeza jitihada zaidi kwa kutoa elemu hasa katika maeneo ya vijijini ambako bado wananchi wengi hawana uelewa kuhusu vipimo sahihi, Wajumbe wa kamati wameongeza kuwa WMA iwe na ratiba ya kufanya ukaguzi wa kushtukiza wa mara kwa mara kwa wafanyabiashara na wauzaji wa mazao wasiozingatia sheria na taratibu za vipimo ili kuwabaini wasiofuata vipimo sahihi.

Naye Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Kigahe (Mb) aliishukuru kamati hiyo kwa michango yao mizuri na kuahidi kutekeleza maelekezo yote ya kamati yaliyotolewa kwa lengo la kuleta tija kwenye sekta ya Viwanda na Biashara kwa kumlinda Mkulima na mlaji wa mwisho wa bidhaa mbalimbali hapa nchini.

Kikao hicho ni mwendelezo wa utaratibu wa vikao vya kamati za kudumu za bunge wa kupokea, kujadili na kutoa maelekezo mbalimbali kwenye Wizara na Taasisi zake kabla ya kuanza kwa bunge la mwezi Septemba, 2022.

# Taanzania na Zambia Kuendelea Kushirikiana katika Kukuza Biashara



Tanzania na Zambia zimekubaliana kuendelea kushirikiana katika kuibua fursa za biashara na kutatua changamoto zilizopo na zitakazojitokeza katika ili kukuza biashara na uwekezaji baina ya nchi hizo mbili.

Hayo yamesemwa na Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb) na Waziri wa Biashara na Viwanda wa Zambia Mhe. Chipoka Mulenga walipokutana na kujadiliana kuhusu masuala ya uwezeshaji, biashara na kukuza uchumi baina ya Tanzania na Zambia katika kikao kilichofanyika Agosti 3, 2022, Jijini Dar es Salaam.

Mawaziri hao walikutana kufuatia maagizo yaliyotolewa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Hakainde Hichilema, Rais wa Zambia katika kikao chao kilichofanyika Ikulu Dar es Salaam tarehe 2 Agosti 2022 ambapo waliagiza Mawaziri wa Biashara kukutana mara moja kujadili masuala ya biashara baina ya Tanzania na Zambia.

Dkt. Kijaji ameeleza kuwa miongoni mwa changamoto zinazofanyiwa kazi ni pamoja na ucheleweshaji wa kuruhusiwa magari ya Tanzania katika mpaka wa Tunduma Nakonde, kunyang'anywa pasi za kusafiria kwa wafanyabiashara wadogo na na wizi wa mizigo unaofanywa kwa madereva kutoka Tanzania.

Kwa upande wake Waziri wa Biashara na Viwanda wa Zambia Mhe. Chipoka Mulenga amesema wanafanyia kazi changamoto zilizowasilishwa huku akisisitiza lengo ni kuimarisha biashara ndani ya Afrika.

Katika kikao hicho, Mawaziri walikubaliana kufanya kikao cha pamoja ambacho kitajadili kwa kina masuala ya kibiashara na changamoto zilizopo baina ya Tanzania na Zambia. Waziri wa Zambia aliahidi ndani ya wiki mbili kuwasilisha mapendekezo ya tarehe za kikao hicho na ilikubalika kitanguliwe na kikao cha sekta binafsi.

Aidha Mawaziri hao walisisitiza kuendeleza ushirikiano ambao umekuwepo tangu enzi za Mhe. Mwalimu Julius Nyerere, Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Keneth Kaunda, Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Zambia na sio kwa kushindana.

Vilevile, Mawaziri hao walikubaliana kuendeleza dhamira nzuri ya Waheshimiwa Marais wa nchi zote mbili ya kuondoa vikwazo na kuwezesha biashara na uwekezaji ili kukuza uchumi na hatimaye ajira kwa wananchi wa pande zote mbili.


INDUSTRY
TANZANIA



# Dkt. Abdallah Akagua Utendaji wa Taasisi Zilizo Chini Ya Wizara Katika Maonesho ya Nane Nane 2022 Mkoani Mbeya




Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara Dkt. Hashill Abdallah ametembelea na kukagua utendaji wa taasisi zilizo chini ya Wizara zilizoshiriki maonesho ya kilimo ya nane nane mwaka 2022.

Maonesho ya Wakulima nane nane yamefanyika kuanzia tarehe 01 – 08 Agosti, 2022 ambapo taasisi mbalimbali na sekta binafsi hushiriki katika kutoa elimu ya kazi na shughuli wanazofanya na kueleza ni namna gani shughuli hizo zinashiriki katika kuendeleza biashara hasa kupitia kilimo.

Maonesho ya nane nane kitaifa 2022 yamefanyika Mkoani Mbeya katika Viwanja vya John Mwakangale yakiwa na kauli mbiu ya "AGENDA 10/30 Kilimo ni Biashara: Shiriki kuhesabiwa kwa mipango bora ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi".

# MTAMBO WA KUSAFISHA MAFUTA YA ALIZETI

## (Sunflower Oil Double Refinery Plant)



Unasafisha lita 1000 kwa siku 1. Unatumia umeme wa njia tatu, unaendeshwa na watu 15. Sehemu ya kusafisha pekee inapatikana kwa Tsh 36,545,000.

Gharama za kutengeneza na kuufunga Mtambo pamoja na mitambo ya kuchekecha, kukamua, kuchuja, kuhifadhi na mafunzo ni Tsh 76,500,000.

Kwa taarifa zaidi tembelea www.temdo.or.tz au piga namba 0765 173 400



Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Viwanda na Biashara
S.L.P 2996, 40478 Dodoma,Tanzania Mji wa
Serikali Mtumba, Mtaa wa Viwanda
Telephone: +255 26 2963470
Nukushi: +255 26 2963117
Barua pepe: ps@mit.go.tz gcu@mit.go.tz
www.mit.go.tz